
Somo la 2: Kushauriana Pamoja

Unaweza kufundisha somo hili lote katika ujumla wake au ukaligawa katika sehemu fupi fupi. Tumia somo hili kulingana na hali na mahitaji ya eneo lenu, umri, na uelewa wa urais wa akidi yako au urais wa darasa lako.

NGUVU HUJA KUTOKANA NA KUSHAURIANA KWA PAMOJA

Njia ya Bwana ya kuongoza Kanisa Lake ni kupitia mabaraza (ona [Mafundisho na Maagano 43:8-10](#)). Kushauriana pamoja kunaweza kutusaidia sisi kuwa wamoja kama urais wa akidi au darasa, tukiongozwa na Roho katika kufanya maamuzi, na wenye ufanisi zaidi katika kufanya kazi ya Bwana. Je, ni kwa jinsi gani kushauriana pamoja kunatusaidia sisi kufanya maamuzi yaliyo bora zaidi?

KUSHAURIANA PAMOJA KUNAWEZA KUTUSAIDIA SISI KUPOKEA UFUNUU

Mzee Neil L. Andersen alifundisha kwamba “ufunuo umetawanywa mionganini mwetu” (katika [“Auxiliary Panels Use New Training Library,” Ensign](#), Apr. 2011, 76). Kushauriana kunaturuhusu sisi kuukusanya ufunuo huo tunapokuwa tunapanga na kutekeleza kazi ya Bwana. Ili kulieleza kwa mfano wazo hili, ungeweza kumpa kila mshiriki wa urais vipande vichache vyaa mchezo wa fumbo rahisi na waalike kufanya kazi pamoja ili kukamilisha fumbo hilo.

- Je, ni kwa jinsi gani mfano huu unatumika kwenye kushauriana kama urais?
- Je, kwa nini ni muhimu kwa kila mtu kuchangia katika baraza?
- Je, tunaweza kufanya nini ili kila mtu ajisikie mwenye faraja kushiriki?
- Je, tunaweza kufanya nini ili kumwalika na kumsikiliza Roho Mtakatifu tunaposhauriana pamoja?

Fikiria kuhusu changamoto au hitaji katika akidi au darasa lako. Fanya mazoezi ya kushauriana pamoja kuhusu jinsi ya kuitatua.

NYENZO SAIDIZI

- [Mathayo 18:20](#)
- [Etheri 2:14-3:16](#)
- [Mafundisho na Maagano 88:122](#)
- [Mafundisho na Maagano 107:84-87](#)
- M. Russell Ballard, [“Strength in Counsel,” Ensign](#), Nov. 1993, 76–78
- [Kitabu cha Mwongozo: Kuhudumu katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho](#), [10.4, 11.3.4](#), ChurchofJesusChrist.org